

**Swahili transcript:**

Kuhusu usafiri Tanzania, tuna usafiri wa aina nyingi, kwa hiyo karibuni sana Tanzania kwa vile hamtapata taabu ya usafiri. Aah! Nikianzia katika miji mikubwa kwa mfano jiji la Dar es salaam, katikati ya jiji kuna usafiri mwingi sana, na usafiri wa mabasi na tunaita daladala. Kwa hiyo hizi daladala zinazunguka katika mitaa mbalimbali na maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es salaam. Kwa hiyo usafiri wa daladala ni mzuri na asilimia kubwa ya wakazi wa jiji la Dar es salaam wanatumia usafiri huu wa daladala, kwa sababu pia ni rahisi ukilinganisha na usafiri mwingine kama wa kuchukua taksi. Vilevile kuna maeneo mengine ambayo daladala hazifiki kwa hiyowatu ambao wanakwenda maeneo kama hayo huwa wanakodi taksi, kwa hiyo pia kuna usafiri mwingi wa taksi kwa hiyo inategemea na eneo ambalo unakwenda, kwa hiyo katika maeneo yote utafika vizuri, sehemu ambazo daladala zinafika utafika vizuri, na sehemu ambazo daladala hakuna, basi wakazi wa jiji hili la Dar es salaam pamoja na maeneo mengine ya mikoa mingine ya Tanzania wanatumia pia usafiri wa taksi. Ukichukulia hata mfano jiji la Arusha, na Mwanza, Dodoma, Iringa, Mbeya kote pia kuna usafiri huu wa daladala ambazo zinakuwa zinazunguka maeneo mbalimbali pale mjini, na sehemu nyingine kama daladala haifiki, basi aah! Wakazi wale ambao wanataka kufika maeneo hayo huwa wanakodi taksi. Na nikizungumzia kwa upande wa Dar es Salaam hasa kwa sababu nimeishi hapo, aah! mara nyingi usafiri huu wa daladala ndio ambao ni mzuri na unawasaidia watanzania wengi kwa sababu nauli yake pia ni ndogo ukilinganisha na usafiri wa taksi. Kwa hiyo na jinsi gani hizi daladala zinafanya kazi ni kwamba hakuna muda maalum labda kwa mfano aah! Mtu labda anatoka maeneo labda ya Mwenge, kuna eneo linaitwa Mwenge Dar es Salaam, kwa mfano anatoka Mwenge na anataka kwenda Posta mpya, Posta mpya ndio eneo ninaweza nikasema ndio katikati ya jiji, na ndio sehemu ambayo ni kubwa na ofisi nyingi za kiserikali na ofisi binafsi zipo kule na unapata mandhari nzuri sana ya bahari ya Hindi pamoja na ni sehemu nzuri sana na inavutia na inapendeza sana, kwa hiyo kwa mfano mtu anatoka Mwenge anakwenda Posta, ni kwamba usafiri upo muda wote, hakuna ule muda kusema labda basi la Mwenge kwenda Posta mpya labda litafika baada ya dakika tano au dakika kumi, hapana, kule unapotaka kwenda sehemu yoyote ni muda

ule unaotaka kwenda ndio unapanda daladala. Ni tofauti na hapa Marekani nimeona kwamba ukitaka kusafiri lazima uwe na ratiba, ratiba ya basi. Kwa sababu kama huna ratiba ya basi, unaweza ukakaa muda mrefu kituoni na usijue basi linakuja saa ngapi, kwa hiyo kwa hapa Marekani ni kwamba lazima uwe na ratiba ile ya usafiri wa basi kwamba unajua basi linalotoka labda chuo cha Smith, litafika chuo cha Massachusetts saa ngapi, na kama unataka kwenda chuo cha Amherst, kwa hiyo ni lazima ujue ratiba ya basi. Lakini kwa Tanzania hakuna ratiba, hakuna watu hawatembei na ratiba kwamba nataka niende Posta au nataka niende Mwananyamala, au nataka niende Kimara, au nataka niende Mbezi Beach, aaah! Hakuna ratiba ya mabasi kwamba wakati ule ambao unataka kwenda ndio wakati huohuo unaenda unapanda gari.

**English translation:**

In Tanzania, we have many means of transportation. Welcome to Tanzania, because you will not have any problem with transportation. Starting with big cities like Dar es Salaam, we have public transportation which we call *daladala*. These buses (*daladala*) have several routes around the streets of the city. *Daladala* transportation is good. The majority of Dar es Salaam inhabitants use this kind of transportation. The *daladala* is cheap compared to other forms of transportation, such as a taxi. In some areas where *daladala* is not in operation, people somewhere use taxis. So it depends on where you are going. You can use the *daladala* or a taxi; there is no problem with transportation. We use these kinds of transportation in all parts of the country. In regions like Arusha, Mwanza, Dodoma, Iringa and Mbeya, they use *daladala*. These *daladala* pass throughout the cities and other places. In other places where *daladala* transportation is not operating, they use taxis. I have lived in Dar es Salaam for years and have found that many people prefer *daladala* because it is cheap. It helps many Tanzanians because it is affordable compared to taxis. There is no time limit to access *daladala* transport. For example, if someone is at Mwenge<sup>1</sup> and wants to go to Posta Mpya,<sup>2</sup> or if you are at Mwenge and want to go there, you can take a bus right away. You do not have to wait for

---

<sup>1</sup> The name of a place in Dar es Salaam.

<sup>2</sup> Another place in Dar es Salaam, where you can find many government and private offices as it used to be the city center, where you can view the Indian Ocean.

several minutes. Let's say, a bus might come after five or ten minutes? Not so! Wherever you want to go, at any time, buses are always there. It is different from here in America, when, if you want to go somewhere, you need a bus schedule. If you do not have a bus schedule, you can wait at the bus stop for long time not knowing when the bus will arrive. Here in America, you have to have a bus schedule. For example, the bus from Smith College will arrive at the University of Massachusetts at such and such a time, and if you want to go to Amherst College, you should know at what time you need to take a bus. But in Tanzania, we do not have bus schedules. If you want to go to Posta, or Mwananyamala, or Kimara, or Mbezi Beach, the exact time you want to go, you just go and take a bus.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated